JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU




KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.







**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshiriki katika maadhimisho ya siku ya Mashujaa katika Uwanja wa Mashujaa uliopo Mtumba Jijini Dodoma.**



Rais Mwinyi ajionea mifumo mbalimbali banda la Ofisi ya Waziri Mkuu Sabasaba

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi leo tarehe 07 Julai, 2025 ametembelea Banda Jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu lililopo katika Maonesho ya 49 ya Biashara (SABASABA) yanayoendelea Jijini Dar es Salaam.

Katika banda hilo, Dkt. Mwinyi ameona mifumo mbalimbali ikiwemo Mfumo wa Ramani za Vihatarishi vya Maafa Vinavyotokana na Mabadiliko ya Tabianchi umeandaliwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 31(2)(a) cha Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura ya 242 kinachotoa wajibu kwa Wizara, Idara, taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa, na mamlaka za Serikali za mitaa kujumuisha katika mipango na bajeti zao hatua za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga na kujiandaa kukabiliana na maafa.

Mfumo huo unatoa taarifa za vihatarishi vya maafa kwa kutumia teknolojia ya mifumo ya taarifa za kijiografia zinazowezesha utambuzi wa maeneo yaliyo katika hatari zaidi ya kuathirika na majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi kama mafuriko, ukame na ongezeko la joto. Kwa kuzingatia viashiria vya kijamii, kiuchumi, kimazingira na kiteknolojia.

Lengo la mfumo huo ni kusaidia taasisi za serikali, sekta binafsi, mashirika ya maendeleo na wadau wengine kutumia ipasavyo ramani hizo katika upangaji na utekelezaji wa mipango na mikakati katika uendelezaji wa miundombinu, usimamizi wa matumizi ya ardhi na shughuli za kiuchumi.

Aidha, Dkt. Mwinyi ameelezwa kuhusu mfumo wa taarifa ya haraka dhidi ya moto, mfumo unaolenga kushughulikia changamoto ya ucheleweshwaji wa taarifa kuwafikia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutokana sababu mbalimbali ikiwemo kutofahamu namba ya dharura na taharuki pindi tukio la moto linapotokea, vilevile katika maeneo yenye vikwazo vya matumizi ya simu za mkononi kama vile mashuleni na magereza.

Mfumo huo umeunganishwa moja kwa moja na mtungi wa kuzimia moto, ambapo mara mtungi unapochukuliwa kwa ajili ya kudhibiti moto, mfumo hutuma taarifa ya tahadhari kwa njia ya simu na ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) ukionesha eneo la tukio kwa Jeshi la Zimamoto na wadau husika bila kuhitaji uingiliaji wa binadamu.

Vilevile, Rais Mwinyi ameelezwa kuhusu Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za Watu Wenye Ulememavu ambapo ni programu ya kielektroniki inayojumuisha Usajili wa Watu wenye ulemavu, Hifadhi salama ya Taarifa za Watu wenye ulemavu pamoja na Kuhamisha Taarifa za Watu wenye Ulemavu.

Aidha, faida za mfumo huo unalenga kupunguza gharama za usafiri na vifaa kwa ajili ya usafiri, kutoa takwimu sahihi zinazosaidia serikali, kupanga na kutekeleza sera kwa ufanisi na kuongeza ujumuishaji wa watu wenye ulemavu kwenye huduma za kijamii na maendeleo.

Rais Mwinyi ametembelea banda hilo kama Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Saba Saba yanayofanyika katika viwanja vya Sabasaba, Kilwa Road, Jijini Dar es Salaam.

.





# Wakandarasi kamilisheni ujenzi wa majengo ya Serikali Mtumba - Waziri Lukuvi

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. William Lukuvi ameipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutekeleza kikamilifu maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa Wizara ya kwanza kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi na kuwezesha Idara na Vitengo vyake kuhamia Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.

Waziri Likuvi ametoa pongezi hizo leo alipotembelea Wizara hiyo kwa lengo la kukagua ujenzi wa Majengo ya Serikali ambao ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu ya Serikali kuhamia Dodoma.

Mhe. Lukuvi amesema kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii licha ya kukamilisha mapema ujenzi wa jengo hilo, inastahili pia kupongezwa kuwa wa kwanza kuhamia na kuwa mfano katika Matumizi ya samani za Ofisini zilizozalishwa hapa nchini kupitia mazao ya Misitu.

"Ninyi ni mabalozi wazuri wa Matumizi ya bidhaa zetu za hapa nchini zinazotokana na Misitu yetu, niimani yangu kuwa Wizara zote zitaiga mfano huu". Aliongeza Mhe. Lukuvi.

Aidha Mhe. Lukuvi ametoa rai kwa watumishi wa Wizara hiyo kuhakikisha wanatunza vyema miundombinu na vifaa vilivyopo ili viweze kudumu kama ilivyo kusudiwa.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Dkt. Hassan Abbasi amemshukuru Waziri Lukuvi kwa ziara yake, na kuahidi kuwa Wizara itatekeleza vyema maelekezo aliyoyatoa hususani ya usimamizi mzuri wa Matumizi ya jengo na vifaa vilivyopo.





Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa William Lukuvi ameonya Wakandarasi wanaosuasua kukamilisha ujenzi wa Majengo ya Wizara na Taasisi katika Mji wa Serikali Mtumba licha ya serikali kutoa fedha.

Waziri Lukuvi ameyasema hayo hii leo Jijini Dodoma alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa majengo hayo ambayo yanagharimu Sh. biloni 738.

Ameagiza kuhakikisha wanakamilisha ujenzi huo kabla ya Oktoba mwaka huu ili watumishi waweze kuhamia na kutoa huduma kwa wananchi.

Waziri Lukuvi amebainisha kuwa hakuna kisingizio cha kusuasua kwa ujenzi huo kwani Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ametoa fedha kwa ajili ya kukamilisha.

"Wasukumeni wakandarasi wanaosuasua kukamilisha ujenzi wa kudumu wa ofisi za wizara na taasisi ili watumishi wote wahamie na watoe huduma kwa wananchi, kama ilivyotakiwa na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa urahisi na wepesi," amesisitiza Mhe. Lukuvi.

Aidha, ameongeza kuwa, "Tunatamani baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu wizara zote ziwe zimehamia Mtumba ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Katika hatua nyingine Lukuvi amezipongeza wizara ambazo tayari zimeshahamia licha ya majengo yao kutokukamilika ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## Dkt. Yonazi awaasa watumishi Ofisi ya Waziri Mkuu kuongeza bidii katika kutekeleza majukumu yao.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi amewaasa Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi mkubwa katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Ameyasema hayo wakati akifungua Mkutano na Watumishi wa Ofisi hiyo ambapo alisema kuwa ni muhimu kuwa na nidhamu ya kazi, kushirikiana na kuendelea kuwa wabunifu katika majukumu ya kila siku, na kuwakumbusha watumishi kuwa kazi wanazofanya zinagusa maisha ya mamilioni ya wananchi, hivyo ni wajibu wa kila mtumishi kuhakikisha anatoa huduma bora na kwa viwango vya juu.



“Pia, nawasihi kuendelea kujenga mshikamano miongoni mwenu. Tunaposhirikiana, tunajenga nguvu ya pamoja ambayo hakuna changamoto inayoweza kutuzuia. Nawaomba tuendelee kufanya kazi kwa bidii na kwa moyo mmoja. Kumbukeni kuwa, kila mchango wenu una thamani kubwa katika kufanikisha malengo ya Ofisi yetu na Taifa kwa ujumla.” Alifafanua Dkt. Yonazi.

Katibu Mkuu Yonazi aliendelea kusema kuwa, katika kuboresha Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kushughulikia changamoto zinazohusu mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kukuza ubunifu katika utendaji kazi wa kila siku na kuimarisha mifumo bora zaidi ya kufuatilia maendeleo ya kazi na kuhakikisha kila mfanyakazi anawajibika ipasavyo kwa nafasi yake.

Katika Mkutano huo watumishi wataweza kupata Elimu kutoka kwa wataalam wa Mfuko wa Uwekezaji wa UTT kuhusu umuhimu wa kuwekeza, pamoja na mambo mengine pia watapewa elimu itakayowakumbusha masuala mbalimbali yanayohusu uzingatiaji wa maadili ya utumishi wa umma, masuala ya Afya hususan homa ya ini na magonjwa yasiyoambukizwa.



.



Dkt. Yonazi Aipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu maonesho sabasaba

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi amewapongeza watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwa maendeleo ya Taifa.

Dkt. Yonazi ameyasema hayo leo Ofisini kwake jijini Dodoma akikabidhiwa tuzo na Mkurugenzi wa Idara ya Uwezeshaji Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi Bw. Conrad Milinga iliyotolewa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati akifungua Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam Sabasaba 2025.

Alisema Ofisi ya Waziri Mkuu kupokea tuzo kumeongeza motisha katika ushiriki wa maonesho yajayo makubwa ya Kimataifa ya Sabasaba na kutambua mchango wa Ofisi hiyo iliyoutoa kwa wananchi katika kipindi chote cha maonesho hayo na kutambua huduma ianayotolewa kwa wananchi.

"Ofisi ya Waziri Mkuu imefurahi sana kupokea tuzo hii kama ishara ya kutambua ushiriki wetu na mchango ambao Ofisi yetu inatoa kwa wananchi hivyo tunaamini ushiriki wetu unaofuata utakuwa wa viwango vya juu sana," Alisema Dkt. Yonazi.



# Tanzania Yatangaza Utayari wa Kuandaa Mashindano ya CHAN

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dkt. Jim Yonazi, amesema kuwa Tanzania ipo tayari kwa ajili ya kuandaa Mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), yatakayoanza rasmi Agosti 2, 2025.

Akizungumza mara baada ya ziara ya ukaguzi wa miundombinu ya michezo jijini Dar es Salaam, Dkt. Yonazi alisema maandalizi yamefikia hatua nzuri na viwanja viko tayari kwa mashindano hayo makubwa.

Akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Makatibu Wakuu ya CHAN na AFCON, Dkt. Yonazi alitembelea viwanja vya Benjamin Mkapa, Isamuhyo, Shule ya Sheria na Gymkhana, akisisitiza kuwa Serikali imejipanga kuhakikisha miundombinu yote inakidhi viwango vya kimataifa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Bw. Gerson Msigwa, ametoa wito kwa Watanzania kuonesha uzalendo kwa kujitokeza kwa wingi viwanjani kuishangilia Taifa Stars.



# Dkt. Kilabuko: Ushirikiano wa kikanda muhimu kukabili maafa ya kibinadamu

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dkt. James Kilabuko amehimiza ushirikiano wa kikanda katika kukabiliana na majanga ya kibinadamu yanayochochewa na mabadiliko ya hali ya hewa, kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa kitaalamu na kuimarisha vituo vya ufuatiliaji wa majanga na tahadhari ya mapema (Situation Room).

Akizungumza leo wakati wa ufunguzi wa mafunzo maalum ya kubadilishana uzoefu, yaliyoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na UNDRR na Kituo cha Sayansi cha Afrika Magharibi kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (WASCAL), Dkt. Kilabuko alisema mafunzo hayo ni sehemu ya kuimarisha uwezo wa kanda katika kukabili matukio ya majanga.

.

Mafunzo hayo yalihusisha ujumbe kutoka Ghana, Togo na Burkina Faso. Dkt. Kilabuko alieleza kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa majanga, kupitia vituo vyenye uwezo wa kukusanya taarifa mbalimbali, zikiwemo za hali ya hewa, maji, kijamii na kiuchumi, jambo linalosaidia kukabili majanga kama vile ukame na mafuriko.

"Tunauzoefu mkubwa wa kiutendaji ambao unasaidia kuhakikisha vituo vyetu vinafanya kazi kwa ufanisi kwa kuratibu taasisi mbalimbali kukabiliana na majanga," alisema Dkt. Kilabuko.

.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na
kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.





KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480